**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA(FUNGU 44) KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016.

Ofisi ya Bunge,
S. L. P 941,
**DODOMA**
Mei, 2015.

# 1.0 TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA(FUNGU 44) KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016.

## 2.0 1.0 UTANGULIZI:

## 3.0

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) ya Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara(Fungu 44) kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea Taarifa kuhusu utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Viwanda na Biasharapamoja na mashirika yaliyo chini ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2014/2015 na Makadirio ya Bajetiya wizara hiyo kwa mwaka wa Fedha 2015/2016. Kamati ilipata fursa ya kuchambua na kujadili kwa kinamafanikio na changamoto za

utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Viwanda na Biashara;na hatimaye kuishauri Wizara hiyo ipasavyo.


**Mheshimiwa Spika,**pamoja na kuwepo changamoto mbalimbali, kwaujumla Kamati inaridhishwa na mafanikio yanayopatikana katika sekta ya Viwanda, Viwanda vidogo na Biashara ndogo, Sekta ya Masoko na Sekta ya Biashara. Aidha, mafanikio yaliyopatikana yamechangiwa na umakini wa Wizara katika upangaji wa vipaumbele vyenye kuleta matokeo ya haraka kisekta; na hali kadhalika kuzingatia na kutekeleza maagizo na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA NA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015.

### 2.1 WIZARA

**Mheshimiwa Spika,**Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ilitengewa shilingi bilioni 111,958,354,000 kati ya hizo shilingi bilioni 33,356,643,000 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 78,601,711,000 ni matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia April, 2015 Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 93,185,222,288 sawa na 82% ya fedha zilizotengwa ikiwa shilingi bilioni 27,905,758,188 ni za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 65,279,464,100 ni za matumizi ya maendeleo.

*Kielelezo 8:Bajeti iliyopitishwa kwa mwaka 2014/2015 ikilinganishwa na fedha zilizotolewa hadi kufikia Aprili, 2015*




## 2.3 Utekelezaji wa Malengo ya Wizara 2014/2015

**Mheshimiwa Spika,**Wizara katika kuendeleza Sekta ya Viwanda kwa Mwaka 2014/2015 imeweza kuendeleza Utekelezaji wa mkakati unganishi wauendelezaji Viwanda nchini kwa kuendesha uhamasishaji wa uwekezaji hususani kwa Viwanda vinavyoongeza thamani ya mazao ya kilimo kwa kuendeleza Viwanda Nchini ili kuongeza mauzo ya ngozi, nguo na mavazi.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia mkakati huo imesimamia utekelezaji wa ***Mpango Kabambe wa kuendeleza Viwanda*** (Master Plan) kwa kufufua na kuongeza viwanda vingine vya ngozi, viwanda vya nguo na mavazi. Aidha, kiwanda kipya cha DAHONG kilichopo Shinyanga kitawezesha kuinua wakulima wa Pamba na kukuza uzalishaji katika Sekta ya Nguo na Mavazi.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imebuni kuanziasha mpango wa kitaifa wa Useketaji (hand loom weaving), waseketaji 23 wanawake wamefuzu mafunzo hayo ya useketaji na kupatiwa nyenzo za kuanza uzalishaji wa kibiashara. Na kikundi kingine cha waseketaji 24 kimeanza mafunzo hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Mpango huo imelenga kufundisha kati ya Waseketaji 1,872 ifikapo 2020 kwa ajili ya kukuza Sekta hii ya Uzalishaji wa Nyuzi kwa ajili ya uzalishaji wa Nguo na Mavazi.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara katika utekelezaji wa mkakati wa Sekta ya Nguo na Mavazi nchini, imeweka mwongozo wa Uwekezaji (*Investment Guide for the Textile and Garment Sub-Sector*), na kuainisha vivutio mbalimbali vya Uwekezaji vilivyopo nchini na kuviweka katika tovuti (***www.tdu.or.tz***), kutembelea viwanda vyote ili kubaini changamoto zinazo wakabili na kutoa ushauri mfano katika upande wa matumizi bora ya Umeme na matumizi ya gesi na n.k.

**Mheshimiwa Spika**, Viwanda vya Ngozi nchini kwa sasa vipo saba ambavyo husindika ngozi kwa hatua ya *Wet Blue,* na vinauwezo wa kusindika futi za mraba milioni 110 kwa Mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ikishirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi zinaandaa mkakati mpya wa kuendeleza zao la Ngozi ambao utalenga zaidi uongezekaji thamani ya ngozi (Lether Value addition strategy) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato(TRA), kwa lengo la kuliingizia taifa mapato kwa kukusanya kodi katika ngozi inayouzwa nje na bidhaa kamaa vile viatu, mabegi kwa mujibu na sheria ili kulinda viwanda na Sokola ndani dhidi ya bidhaa za ngozi zinazoingizwa kutoka nje.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka 2014/2015 Wizara kwa kushirikia na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia imewezesha kupatikana kwa Usajili kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) wa Chuo cha Teknolojia Dae es salaam ili kuanza kutoa mafunzo ya Stashahada ya Taaluma ya Ngozi (Ordinary Diploma in Leather Technology).

**Mheshimiwa Spika,** Chuo kilianza kutoa mafunzo ya teknolojia ya utengenezaji wa viatu kwa njia ya mtandao na jumla ya washiriki 88 kutoka mikoa 10 walipata mafunzo na kupata Shahada (Certificate) katika kozi hiyo ya kompyuta (IT FUNDI). Aidha, Chuo kimeweza kuunganishwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili kuongeza kasi na ufanisi katika kutoa

mafunzo ya teknolojia ya viatu na Teknolojia ya habari na Mawasiliano (TEHAMA)

**Mheshimiwa Spika,**Wizara katika lengo la kutoa mafunzo ya kuongeza tija, ufanisi na ubora wa bidhaa kwa wenye Viwanda katika kupitia programu ya ***KAIZEN*** kwa kushirikiana na Shirika la Misaada la Japan (JIKA) pamoja na UNIDO, jumla ya Viwanda 42 vilivyopo katika mikoa ya Dar es Saalam, Morogoro na Dodoma vimejiunga na Mradi huu wa ***KAIZEN*** na kupata mafunzo ya nadharia na vitendo.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu pia umeanzisha uhusiano wa Kimataifa wa kupeana taarifa za kimaendeleo ya mradi kwa nchi zilizotumia dhana hiyo mfano ni Kenya na Sri Lanka.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imeshiriki kikamilifu katika kuandaa Mpango Kazi wa Sera ya Viwanda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo Mpango kazi huo umekamilika na utekelezaji wake umeanza. Aidha, Wizara imeshiriki katika kuandaa Rasimu ya Mpango Kazi na Mpango wa Utekelezaji wa Nguzo ya Maendeleo ya Viwanda kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa SADC. Rasimu imekamilika na inasubiri kupitishwa na Baraza la Mawaziri wa Biashara wa SADC(CMT).

Mheshimiwa Spika, Wizara imewezesha kupatikana kwa mfuko wa Dhamana wa mikopo ISME Credit Gurantee Scheme) kwa Wajasiliamali wadogo na wakati katika sekta ya Uzalishaji hususani usindikaji wa mazao ya kilimo na Mifugo. Mfuko utarahisisha upatikanaji wa mitaji kwa

wajasiliamali wadogo na wakati. Mtaji wa Mfuko huu umetolewa na mfuko wa pamoja kati ya Serikali ya Tanzania na Japan (Tanzania- Japan Food Aid Counterpart Fund na Japan International Cooperation Agency)

## 2.4 SEKTA YA BIASHARA (MAUZO/MANUNUZI NA UBORESHAJI MZINGIRA);

**Mheshimiwa Spika;**Wizara katika kuendeleza kupanua wigo wa fursa za masoko kwenye masharti nafuu ili kuvutia biashara na Wawekezaji wameweza kufanya majadiliano ya kibiashara kati ya Nchi (Bilateral), Kikanda (Regional) na Kimataifa (Multilateral), ambayo yanafanyikaa chini ya WTO,
EAC, SADC, Indian Ocean Rim- IOR na yale yanayohusu mpango wa AGOA.
**Mheshimiwa Spika,** Wizara katika kipindi cha 2014/2015 imeendelea na juhudi za kutafuta fursa za masoko na Uwekezaji baina ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa. Aidha, Wizara kupitia majadiliano ya nchi na nchi imeshiriki Kongamano la III la Biashara baina ya Tanzania na China mwezi wa Novemba, 2014 mjini Beijing China.

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania Ilipata fursa ya kunadi vivutio na fursa za Biashara na Uwekezaji kwa wafanya Biashara wa China. Aidha, Serikali ya Tanzania ilifanikiwaa kusaini Mkataba wa Biashara na China ambapo kupitia makubaliano hayo China iliongeza idadi ya bidhaa zitakazoingia katika Soko lake kutoka 95% hadi kufikia 97%.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara imeshiriki katika kongamano la biashara lililofanyika mjini Amaan, Jordan Desemba,

2014. Katika kongamano hilo jumla ya makampuni 21 kutoka Jordan yameonesha nia ya kuwekeza Tanzania katika Sekta za kilimo, Dawa za Binaadamu na Mbolea. Aidha, Jordan inategemea kusaini Mkataba wa Ushirikiano wa Biashara na Uchumi na Serikali ya Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutafuta fursa za masoko ya upendeleoyakiwemo ya EAC na SADC, aidha Wizara inashirikiana na taasisi mbalimbali za Serikali na Sekta Binafsi ili kufanya mapitio ya Sheria ya Uasili wa Bidhaa (Rules of  Origin) ya Jumuiya ya Afrika mashariki. Mapitio hayo yalihusu Sekta ya Viwanda na Nguo kwa Bidhaa ya Pamba(Textile Industry), Tumbaku, Samani, Waunganishi wa Magari; na Dawaambapo mapendekezo ya Tanzania yaliwasilishwa Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na bado yapo katika Mchakato katika Baraza la Kisheria na Mahakama na baada ya hapo yataanza kutumika.

**Mheshimiwa Spika,** katika majadiliano ya Kikanda Wizara imeendelea kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kuanzisha eneohuru la utatu (Tripatriate) linalojumuisha kanda za COMESA,EAC na SADC. Aidha, mambo muhimu katika majadiliano haya ni pamoja na kukubaliana kupunguziana ushuru, na utungwaji wa kanuni itakayo tumika kuanzia pale kanda husika itakapofikia viwango/matakwa ya kanuni (Principle of the acquis).

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimaarisha Vituo vya biashara vilivyopo nje ya nchi, (London na Dubai) ili kuendelea kutangaza bidhaa za Tanzania na fursa mbalimbali na kuvutia wawekezaji na Utalii nchini.

## 2.5 CHANGAMOTO ZA WIZARA

Mheshimiwa Spika, Wizara inakabiliwa na Changamoto kama ifuatavyo:

i. Haikuweza kufanya utafiti juu ya bidhaa tano muhimu za Tanzania kutokana na ufinyu wa fedha. Aidha, Wizara bado ina nia ya kutimiza lengo kwa kuendelea

ii. kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha ili kuwawezesha Wazalishaji kuzalisha kwa tija na kuwa na uhakika wa masoko.

iii. Ufinyu wa bajeti katika Vituo vya biashara vya Dubai na London, na hivyo kushindwa kutimiza azma yake ya utekelezaji wa majukumu yake vizuri kama ilivyopangwa

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri vituo vya Biashara kuongezewa Fedha na zifike kwa wakati ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi. Aidha ufanisi huo utasaidia kutafuta masoko kwaajili ya bidhaa zetu na mazao, ambayo yatafanikisha kuingiza fedha za kigeni hapa nchini;

## 2.6 Sekta ya Masoko (Sera, Sheria na Miundombinu)

**Mheshimwa Spika,**katika kukuza masoko, Wizara imeendelea kutekeleza Sekta ya masoko ya Mazao na Bidhaa za kilimo, Kuboresha mazingira ya biashara kwa kupitia Sheria na kanuni, kuimarisha mifumo ya utoaji huduma na usimamizi wa Sheria za biashara, kuendeleza miundombinu ya masoko hususani masoko ya mipakani, maghala, barabara za vijijini na minada ya mifugo na

kuanzisha vituo vya pamoja vya ukaguzi vya mipakani (One Stop Border Post- OSBP).

**Mheshimiwa Spika,**Wizara ikishirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Handeni na Mji wa Makambako pamoja na Benki ya Rasilimali (TIB) imejizatiti kufanikisha ujenzi wa masoko ya kimataifa katika maeneo hayo. Halmashauri hizo zipo katika hatua ya mwisho za kuingia Mkataba na TIB ili kufanikisha ujenzi wa masoko hayo. Aidha, Wizara imefanya upembuzi yakinifu, imeandaa mpango kabambe (*Master Plan),*na kufanikisha uhakiki wa athari ya Mazingira katika ujenzi wa masoko haya. Eneo lingine la ujenzi wa soko la kimataifa lipo Halmashauri ya Kibondo lenye eneo la Ekari 149.7 na tayari limeshafanyiwa makadirio ya gharama za ujenzi.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara katika kuboresha utendaji kazi wa Kamati za Pamoja mipakani JBC nchini, ilikabidhi vifaa kwa ajili ya matumizi ya Ofisini (Samani na Kompyuta) kwa viongozi wa JBC za Tunduma na Rusumo Mei, 2014.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kupitia BRN, Wizara kupitia BRELA inaendelea kuandaa mfumo wa usajili wa makampuni kwa njia ya mtandao (Online registration) ambao utarahisisha usajili mwa makampuni na majina ya biashara na kupunguza muda na gharama za usajili makampuni na majina ya biashara. Aidha, mfumo huu utarahisishanakuboresha Mazingira ya kazi;nahivyo

kuwezesha kazi kufanyika kwa haraka na kwa ufanisi mkubwa bila usumbufu.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia mfumo huu inafanya maandalizi ya kutoa leseni za biashara kwa njia yamtandao wa kompyuta (Online business lincensing) kwa kuanzisha dirisha la Biashara la Taifa (National Business Portal) ambalo litawezesha wafanyabiashara kuomba leseni za biashara kwa kutumia mfumo wa kompyuta.

**Mheshimiwa Spika,** Wafanya Biashara pia watapata taarifa za usajili wa makampuni, majina ya biashara, hataza, leseni za viwanda na leseni za biashara, TIN, VAT na huduma nyingine zinazohitajika katika uanziashwaji wa biashara kwa njia ya mtandao na hivyo kuwa na kituo kimoja (Single window/ one shop centre). Aidha kupitia kituo kimoja, huduma zote za usajili, vibali, vivutio vya uwekezaji na leseni za biashara zitakuwa zinazotolewa na Serikali kwa wafanya biashara.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imekamilisha marekebisho ya Sheria ya usajili wa Shuguli za biashara (Business activities Registration Act-BARA) kama ilivyopendekezwa na wadau hususani Sekta binafsi ikishirikiana na ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, Wizara imeandaa hati na muswada wa marekebisho ya Sheria hii na kuwasilisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa hatua zaidi.

**Mheshimiwa Spika,**Kamati iliarifiwa kuwa katika kuhakikisha haki la mlaji zinalindwa, Wizara imeandaa Sera

ya Taifa ya Kumlinda Mlaji (National Consumer Protection Policy), na rasimu yake (zero draft) imekamilika. Aidha, ili kufanikisha maandalizi ya Sera hii, Wizara imepanga kuendelea na ukusanyaji wa maoni ya wadau pindi fedha za kugharamia zoezi zitakapo patikana.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia ukuaji wa kasi wa teknolojia na mabadiliko makubwa katika mifumo ya kibiashara,Kamati inaona kuwa kuna uhitaji mkubwa na waharaka wa kuwa na Sera ya Taifa ya kumlinda mlaji na madhila ya mfumo wa kibiashara usio wa haki; ambao huhatarisha afya, usalama, na kuleta athari za kiuchumi kwa walaji.

Aidha, uwepo wamtawanyiko wa sheria zinazotumika kumlinda mlaji unaleta changamoto nyingi katika kusimamia sheria hizo; na hivyo kusababisha walaji kushindwa kudai haki zao pindi wanapokumbwa na madhila ya"unfair treatment au poor transactions". Kamati inashauri kuwa Sera inayoandaliwa ijielekeze katika kuhakikisha inaweka mazingira ya kuwa na sheria moja inayounganisha masuala yote yahusuyo haki za walaji.

Kwa hali ilivyo sasa walaji wengi hawajui wapate wapi ushauri au wapeleke wapi malalamiko/madai yao pindi wanapopata matatizo.

Tunashuhudia matangazo mengi yakibiashara yaliyojaa udanganyifu na upotoshaji unaowasababishia walaji usumbufu na hasara kubwa kifedha, ununuzi huduma na

bidhaa hafifu kinyume na matarajio waliyojengewa na wafanyabiashara kupitia matangazo; mfano halisi ni matangazo ya kampuni za simu kwa vifurushi vya muda wa maongezi, vifurushi vya internet “unlimited” ambovyo husababisha kampuni za simu kuendelea kuwakata walaji fedha pindi muda unapoisha ilhali hawajaomba tena kuunganishwa kwenye huduma ya intenet.

## 3.0 UTEKELEZAJI WA MALENGO YA TAASISI CHINI YA WIZARA MWAKA 2014/2015

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na taasisi zilizopo chini ya wizara katika kukuza uchumi wa nchi yetu,taasisi hizi zinakumbwa na changamoto mbalimbali, hususanufinyu wa bajeti, fedha kutokufika kabisa au kufika kwa uchache, rasilimali watu na mambo mengine mengi yanayokwamisha utendaji kazi na ufanisi wa mashirika haya ambayo yana tija kubwa katika ukuwaji wa uchumi nchini.

### 3.1 SHIRIKA LA MAENDELEO LA TAIFA (NDC)

**Mheshimiwa Spika;** takwimu zionaonesha kuwa Serikali ilitenga kiasi cha Shilingibilioni 2.0 kwa ajili ya kuendeleza miradi ya kasi mpya na makaa ya mawe ya Mchuchuma; Shilingi bilioni 3.0kutekeleza Mradi wa Chuma cha Liganga. Taarifa zinaonesha kuwa NDC imekamilisha upatikanaji wa vyeti vya Mazingira vya Mgodi wa Makaa ya Mawe, kituo cha Kufua Umeme, Msongo wa Umeme kutoka Mchuchuma hadi Liganga, Mgodi wa Chuma na Kiwanda cha Chuma. Aidha,  Kampuni imepata Leseni za Uchimbaji wa madini

ya chuma na makaa ya mawe. Aidha Kamati inazo taarifa kuwazoezi la Uthamini wa mali na makazi ya watu ndani ya maeneo ya miradi linatarajiwa kuanza mwezi Mei, 2015 ili kupisha utekelezaji wa mradi. Ukarabati wa barabara zinazoenda kwenye maeneo ya miradi umekamilika ili kuruhusu usafirishaji wa vifaa na mitambo kufikishwa eneo la mradi.

**Mheshimiwa Spika;** kwa upande wa Kiwanda cha kuzalisha Viuadudu vya kuua Viluwiluwi vya mbu waenezao Malaria, Shilingi bilioni 2.906 zilitengwa kukamilisha ujenzi wa kiwanda. Taarifa zinaonesha kuwa ujenzi huu uko katika hatua za mwisho, na kiwanda kinatarajiwa kuanza uzalishaji ifikapo tarehe 30 Juni 2015.

**Mheshimiwa Spika,** NDC imeendelea na jitihada za upatikanaji wa mkopo wa Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia upepo Singida na kuanza ujenzi.Hii ni miongoni mwa jitihada za Serikali katika kuhakikisha inakuwa na vyanzo mbalimbali vya kuzalisha umeme pamoja na kuelekeza nguvu kutumia nishati jadidifu (renewable energy) unatekelezwa na kampuni ya ubia ya *Geo Wind Power Tanzania Limited*. Aidha, Kamati ilijulishwa kuwa Mradi huu ni miongoni mwa miradi iliyoingizwa katika Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (Big Result Now – BRN).

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mkataba wa Mauziano ya Umeme (Power Purchasing Agreement PPA) wa megawati 50 kati ya Geo Wind Power Tanzania Limited na TANESCO

kusainiwa Agosti 2014; na Benki ya EXIM ya China kufanya tathimini na kisha kuridhia kutoa mkopo wa Dola za Kimarekani 136 kwa mkopo kwa riba ya asilimia 2 kwa miaka ishirini (20); Mazungumzo ya Mkataba wa Mkopo (Loan Agreement) kati ya Wizara ya Fedha na Benki ya EXIM yanaendelea kwa kusuasua licha yavibali vyote vinavyohusu

ujenzi wa mradi kupatikana. NDC na wabia wake wako tayari kuanza ujenzi mara mkopo ukipatikana.

***Kamati inasikitishwa na ucheleweshaji huu unaofanyika ndani ya Serikali yenyewe; hasa ikizingatiwa kuwa utekelezaji wa mradi huu ni wa mwaka mmoja tu na utaweza kuingiza megawati za kutosha katika Gridi ya Taifa.***

**Mheshimiwa Spika,**kuhusiana na jitihada zinazoendelea kufanywa na NDC katika kutekeleza hatua za kufufua kiwanda cha General Tyre Arusha ili kuanza uzalishaji wa matairi, hususan jitihada za ukarabati wa mfumo wa umeme; kamati inapongeza hatua iliyofikiwa ya kwa awamu ya kwanza na ya pili. Hatahivyo kamati inatoa angalizo kuwa kwa kuwa kiwanda hiki ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu, ni vyema kasi ya ukamilishaji ukarabati wa umeme wa awamu ya tatu ikaongezeka ili ukarabati wa mitambo na kufanya majaribio ya uzalishaji wa matairi uweze kufanyika mapema.

**Mheshimiwa Spika,**Aidha kwakuwa kiwanda hiki kimekuwa na mgogoro kwa muda mrefu, Serikali ifanye jitihada za makusudi kukamilisha taratibu za manunuzi ya hisa asilimia 26 kutoka kwa mbia wa zamani Continental AG ili kuiwezesha NDC kuendelea kutafuta wabia wenye uwezo na uzoefu wa uzalishaji wa matairi ya magari.

**Mheshimiwa Spika,**Kuhusiana na utekelezaji wa miradi miwili ya kuvuna Magadi katika Ziwa Natron na Bonde la Engaruka, kamati ilifahamishwa kuwa mchakato wa kumpata Mbia kushirikiana kutekeleza mradi unaendelea na uko katika awamu ya mwisho. Kwa maoni ya kamati ni vyema jitihada za makusudi zikafanyika ili kuhakikisha kuwa mbia anapatikana kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha wa 2015. Aidha, Kamati inashauri kuwa jitihada zilizoanzishwa na Shirika kwa kushirikiana na Halmshauri ya wilaya ya Monduli kuainisha mahitaji ya ardhi kwa ajili ya eneo la kiwanda, makazi ya wafanyakazi, shughuli za kijamii pamoja na miundombinu mingine itakayosaidia katika kutekeleza mradizikamilike kwa haraka ili maombi ya kupatiwa ardhi yaweze kuwasilishwa kwa haraka.

**Mheshimiwa Spika,**Kamati inazo taarifa kuwa NDC imekamilisha utafiti yakinifu kwa ajili ya kuanzisha viwanda vya kusindika nyama katika Mikoa ya Arusha, Dodoma na Pwani. Hata hivyo ili utafiti huu uweze kuzaa matunda tarajiwa ni vyema mazungumzo yanayoendelea kwa sasa kati ya NDC na mamlaka mbalimbali kuhusiana na upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya miradi hiyo yakaharakishwa ili kufikia tamati ndani ya kipindi kifupi kijacho

**Mheshimiwa Spika,**Mradi waKasi Mpya wa kuzalisha chuma ghafi, unatekelezwa na kampuni ya ubia ya *Maganga Matitu Resource Development Limited (MMRDL).*Shirika kwa kushirikiana na kampuni hiyo limeendelea na utafiti kwa kiwango cha JORC pamoja na kupata teknolojia muafaka ya kuchenjua chuma.

**Mheshimiwa Spika**, Uchorongaji kubaini wingi na ubora wa chuma na makaa ya mawe umekamilika katika eneo la kilomita za mraba 9.78 kati ya kilomita za mraba 19.55. Utafiti umebaini tani milioni 39.8 zinakubalika kwa kiwango cha kimataifa cha JORC, utafiti zaidi utafanyika ili kubaini kiasi cha rasilimali ya chuma katika eneo lililobaki. Taarifa za awali za uchorongaji zinaonesha kuwepo kwa zaidi ya tani milioni 80 za makaa ya mawe katika eneo la Katewaka. Aidha, Uandaaji wa Taarifa ya uhakiki kwa kiwango cha JORC unaendelea. Kamati inapongeza jitihada hizi na kushauri kazi zaidi kuelekea kwenye uzalishaji kamili iongezeke ili raslimali hii iweze kutoa mchango kwa Taifa.

### *4.1* 3.2 MAMLAKA YA MAENEO HURU YA UZALISHAJI BIDHAA KWA AJILI YA MAUZO NJE YA NCHI (EPZA)

**Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonesha kuwa Serikali katika kutekeleza miradi ya Tanzania Mini Tiger Plan ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 7.0 kwa ajili ya kulipia fidia eneo la Bagamoyo SEZ. Hadi kufikia mwezi Februari 2015 kiasi cha shilingi 6.75 bilioni tayari kilikuwa kimelipwa kwa walengwa katika eneo la Bagamoyo SEZ.Hatahivyo pamoja

na kufanyika malipo hayo, bado shilingi 44.25 bilioni hazijalipwa kutokana na ufinyu wa bajeti.

**Mheshimiwa Spika,**kwa eneo laTanzania-China Logistics Centre – Kurasini, hadi kufikia mwezi Septemba, 2014 Wizara kupitia EPZA ilikuwa imelipa fidia kiasi cha shilingi bilioni 53 kwa watu 538. Aidha kiasi cha fedha kinachodaiwa kumalizia kulipa fidia na malalamiko mbalimbali ya mapunjo yaliyotokana na makosa ya kiuthamini ni shilingi bilioni 3.75.

Aidha, Kamati ilifahamishwa vilevile kuwa Wizara kupitia EPZA imeendelea kulipa fidia kwenye maeneo mengine yaliyofanyiwa uthamini ambayo ni Kigoma SEZ, Tanga SEZ, na Ruvuma SEZyaliyotengwa kwa ajili ya viwanda kwa lengo la kuendelea kukuza sekta ya viwanda hapa nchini kwa kushirikiana na sekta binafsi. Fidia inayodaiwa katika maeneo mengine mpaka mwishoni mwa mwaka wa fedha 2014/2015 ni kama ifuatavyo;Tanga SEZ shilingi bilioni 2.3, Kigoma SEZ shilingi bilioni 1.9 na Ruvuma SEZ shilingi bilioni 2.7.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kwa muda mrefu sasa kamati imekua ikiishauri serikali juu ya umuhimu wa kuhakikisha miradi hii ya kimkakati katika kukuza uchumi inapatiwa fedha za kutosha ili iweze kutekelezwa kwa wakati. Hata hivyo pamoja na jitihada hizi za Kamatibado utekelezaji

umekuwa wa kusuasua. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha inalipa fidia katika maeneo yote yaliyofanyiwa tathmini yaliyopo chini ya EPZ na SEZ kufikia Mwaka wa Fedha 2015/2016; yenye gharama iliyofikia Shilingi Bilioni 60.

Aidha, kwakuwa bajeti iliyowasilishwa na Wizara kwa ajili ya fidia ya maeneo haya ni Shilingi 26 bilioni tu, Kamati inatoa rai kuwa ni vyema Serikali ikatenga Shilingi Bilioni 60 katika fengu hili ili fidia yote iweze kulipwa kwa mkupuo kwa mujibu wa tathmini. Ikumbukwe kuwa:-

- Tathmini hizi zimefanyika muda mrefu tangu mwaka 2008, na kwamba wananchi wamesubiri kwa muda mrefu kupata haki yao ya fidia; na kwa kuchelewa huku gharama zimekuwa zikiongezeka kila mwaka na kuongeza mzigo kwa Taifa
- Miradi kuchelewa kuanza, wawekezaji kusubiri kwa muda mrefu taratibu za kiurasimu husababisha wawekezaji kukata tamaa na hivyo kuamua kwenda kuwekeza kwenye nchi nyingine
- Ni vyema serikali ya awamu ya Nne ikamaliza hatua hii ya ulipaji fidia hii ili Serikali ya awamu ya Tano iingie kwenye utekelezaji wa Miradi.

## *3.3* SHIRIKA LA VIWANGO LA TAIFA (TBS)

**Mheshimiwa Spika,**Licha ya TBS kufanya kazi katika mazingira magumu sana yanayotokana na uhaba mkubwa wa wafanyakazi, Shirika linaendeleza kufanya kazi nzuri ya kuihakikishia jamii ya Watanzania usalama wa Afya zao na kuwakinga na madhila ya umasikini unaoweza

kusababishwa na wafanyabiashara wasio waaminifu. Shirika limeendelea na utaratibu wa kupima ubora wa bidhaa zote mahali zinapotoka kabla ya kuingia nchini (Preshipment Verification of Conformity to Standard–PVoC).

**Mheshimiwa Spika,**Shirika limeendelea na utaratibu wa kupima ubora wa bidhaa zote mahali zinapotoka kabla hazijaingizwa nchini na kutoa vyeti vya ubora (*Certificate of Conformity - CoCs*). Mpaka sasa jumla ya vyeti vya ubora 21,895 vimetolewa. Matarajio ya Shirika kwa mwaka 2014/2015 ni kutoa jumla ya vyeti vya ubora wa bidhaa 32,000 ikilinganishwa na vyeti 26,610 vilivyotolewa mwaka 2013/2014.

**Mheshimiwa Spika**, Shirika linashirikiana kwa karibu na vyombo vingine vya Serikali kama Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA), Mkemia Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Tume ya Ushindani (FCC), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) ili kuhakikisha kuwa bidhaa zinazoingia nchini ni zenye ubora unaokubalika.

Aidha, TBSinashirikiana na SIDO kuhakikisha wajasiriamli wadogo nchini wanazalisha bidhaa bora zinazokidhi ushindani wa kibiashara katika soko la ndani na nje ya nchi. SIDO inawajengea uwezo wa kitaalamu na kiteknolojia na TBS kupitia SIDO inawatambua wajasiriamali hao na kuwapa

huduma za kudhibiti ubora wa bidhaa na kuhakikisha wanapata leseni ya kutumia nembo ya ubora ya TBS. Huduma hii inatolewa kwa gharama ya serikali.

**Mheshimiwa Spika,**TBS inashirikiana na mashirika na taasisi kama CARMATEC, NIT na TCRA katika kufanya shughuli za kuandaa Viwango na ukaguzi wa zana za kilimo na magari yaliyotumika ambayo hayakukaguliwa huko yanakotoka. Katika kuhakikisha kuwa kuna bidhaa zenye viwango, TBS kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, TFDA, TRA, FCC, GCLA na EWURA imekua ikifanya kaguzi za kushtukiza masokoni kuondoa bidhaa zisizokua na viwango na ambazo si salama kwa afya ya mlaji.

**Mheshimiwa Spika**, TBS imeweza kuongeza idadi ya leseni kutoka leseni 100 zinazotarajiwa kwa mwaka 2013/2014 na kufikia leseni 120 katika mwaka 2014/2015. TBS imetoa leseni 130 za nembo ya ubora ya TBS mpaka mwezi Februari 2015, ikiwa ni 108% ya lengo la kutoa leseni 120 kufikia mwezi Juni, 2015. Kati ya leseni 130, leseni 23 zimetolewa kwa wajasiriamali wadogo kwenye bidhaa za mkate, unga wa mahindi, mafuta ya alizeti, mvinyo wa matunda na sabuni.

**Mheshimiwa Spika,** TBS imeongeza idadi ya upimaji sampuli kutoka 10,000 kwa mwaka hadi kufikia 11,000 katika mwaka 2014/2015.Katika kuhakikisha bidhaa zinazoingia sokoni zinakua zenye ubora, Shirika limepima jumla ya sampuli 9,329 kuhakiki viwango vya ubora wa bidhaa hizo, Ikiwa ni asilimia 77.7 ya lengo la kupima sampuli 11,000 kwa mwaka 2014/2015. Aidha, TBS

inatayarisha viwango vya kitaifa vinavyofikia 150 vikiwemo viwango vya sekta ya huduma katika mwaka 2014/2015.

**Mheshimiwa Spika,**TBS imekamilisha kuandaa viwango vya ubora 93 katika kilimo, chakula, uhandisi, kemia, na nguo ikiwa ni asilimia 62 ya lengo la kutayarisha viwango 150 kwa mwaka 2014/2015. Shirika linaendelea kusimamia Viwango vya kitaifa kwa kutumia mifumo ya kuhakiki ubora (*Certification Schemes*).

**Mheshimiwa Spika,** TBS imeendelea na juhudi za kuhakikisha kwamba maabara zote za Shirika zinapata vyeti vya umahiri (laboratory accreditation) ili kuongeza kukubalika kwa bidhaa nyingi za Tanzania katika soko la ndani na la kimataifa. Aidha,Maabara nne (4) za TBS zimepata vyeti vya umahiri.

**Mheshimiwa Spika,**Maabara hizo ni maabara ya ujenzi, maabara ya kemia, maabara ya chakula, na maabara ya nguo. Shirika limefanyiwa tathmini ya awali (*pre-assessment*) katika maabara za Uhandisi kujua mapungufu yaliyopo, ili yaweze kufanyiwa marekebisho kabla ukaguzi rasmi haujafanywa. Maabara ya Kemia imefanyiwa tathmini ya awali kwa lengo la kutanua wigo wa umahiri katika upimaji wa mbolea na mafuta.

**Mheshimiwa Spika,** TBS inatoa mafunzo kwa wajasiriamali nchini kote kuhusu viwango vya udhibiti wa ubora wa bidhaa na kuongeza utoaji vyeti vya ubora wa

bidhaa.TBS imeshirikiana na mfuko wa maendeleo wa Ulaya (EDF) kutoa mafunzo kwa Wajasiriamali Wadogo410 katika sekta ndogo za Chai, Kahawa, Samaki, Mbogamboga, Viungo na Matunda, katika mikoa ya Mbeya, Morogoro, Kagera, Mwanza, Dar es Salaam, Pwani, Mara, Kigoma, Njombe, Tanga, Arusha, Kilimanjaro, Ruvuma, Katavi, Mtwara na Zanzibar. Lengo ni kuwezesha Wajasiriamali wadogo kuzalisha bidhaa bora, Zenye viwango vinavyokubalika kurahisisha upatikanaji wa masoko ya bidhaa hizo.

**Mheshimiwa Spika,**Shirika limeendelea kukagua ubora wa bidhaa mbalimbali ikiwamo magari kabla ya kuingia nchini, kufikia mwezi Machi, 2015 vyeti 31,007 vya ukaguzi wa magari vimetolewa ikiwa ni 73.8% ya lengo la kutoa vyeti vya ukaguzi 42,000 kwa mwaka 2014/2015.

### *3.4* WAKALA WA VIPIMO (WMA)

**Mheshimiwa Spika,**uimarishaji usimamizi wa matumizi ya vipimo vilivyo sahihi nchini kwa kufanya kaguzi mbalimbali kwa zenye lengo la kumlinda mlaji ni jambo muhimu sana. Taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati inaonesha kuwa katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wakala imefanya kaguzi 1,196 nchi nzima sawa na ongezeko la asilimia 84 ikilinganishwa na lengo la kufanya kaguzi 650 mpaka Desemba 2014. Aidha vipimo 303,516 vimehakikiwa sawa na asilimia 45 ya kuhakiki vipimo 673,987 kufikia mwaka 2014/2015.

**Aidha, taarifa inabainisha kuwa** kati ya vipimo 303,516vilivyo kaguliwa, vipimo 286,919 vilihakikiwa (*verified*), vipimo 10,992 vilirekebishwa (*adjusted*), vipimo 567 vilikatazwa kutumika kwa biashara (*rejected*). Sambamba na jitihada hizo, Wakala vilevile ilipima (*calibrate)* matenki 616 na malori ya mchanga 4,422.**Hatahivyo wakati Kamati inapongeza jitihada hizi, inapenda kukumbusha kuwa o**ngezeko kubwa la idadi ya vipimo vilivyokaguliwa kufikia mwaka 2014/2015 limetokana na Wakala kuanzisha huduma ya ukaguzi wa bidhaa zilizofungashwa mipakani. Kamati inashauri jitihada zifanyike zaidi katika vipimo vinavyotumika kwa mazao ya wakulima wetu, na hali kadhalika bidhaa za viwandani ambazo uzoefu unaonesha kuwa hupungua sana ujazo stahiki tangu kutoka viwandani hadi pale zinapowafikia walaji.

**Mheshimiwa Spika,**kuhusianana uimarishaji wa kitengo cha Vipimo Bandarini (WMA Port Unit) ili kiweze kutoa huduma kwa ufanisi; kamati iliarifiwa kuwa Wakala imeajiri watumishi wanne (4) na kupeleka watumishi 14 mafunzo mbalimbali ya muda mrefu na mfupi nje ya nchi katika kozi za *liquid bulk cargo handling*, *Auditing for Oil & Gas*, *Flow measurementand custody Transfer*, *Advanced Gas Chromatoghraphy*, *Oil and Gas Measurement calculation* na *SCADA system*. Kamati inapongeza jitihada hizi, hata hivyo inashauri kasi zaidi ya uimarishaji kitengo; nakuhakikisha unakuwepo usimamizi makini wa eneo hili. Kamati inapenda kukumbusha kuwa udhaifu wowote katika kusimamia vipimo sahihi katika eneo hili unaathari kubwa katika uchumi wa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika, Kuhusiana na**utafiti na uchambuzi wa vipimo vitakavyotumika katika usambazaji wa gesi asilia (*Natural Gas*) na halikadhalika uandaaji Rasimu ya kanuni za usimamiaji wa matumizi sahihi wa vipimo kwenye gesi asilia; Kamati iliarifiwa kukamilika kwa kazi hizi. Aidha kimati ilijulishwa vilevile kuwa tayari Rasimu imesambazwa kwa wadau mbalimabali kupata maoni. Kamati imeridhishwa na hatua hii; hatahivyo inashauri mchakato wa kupata vifaa vya kielekroniki vya mawasiliano vitakavyowezesha kupata takwimu muhimu na sahihi za gesi asilia ukamilike kwa haraka ili Taifa liweze kunufaika na raslimali hii.

**Mheshimiwa Spika,**kuhusiana na umuhimu wa kutungwa kwa sharia mpya vipimo (*Legal Metrology Act*), Kamati iliarifiwa kuwa Waraka unaopendekeza kutungwa kwa sheria mpya tayari umefanyiwa maboresho na Wakala wa Vipimo na tayari umewasilishwa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa hatua zaidi. Kamati inashauri kuwa kutokana na umuhimu wa uhitaji mkubwa wa kuwepo usimamizi mzuri wa uchumi wa gesi; ni vyema Wizara ikafanya kila linalowezekana kuhakikisha kuwa muswada huu unapata nafasi mapema katika bunge lijalo.

## *3.5* CHAMA CHA HAKIMILIKI TANZANIA (COSOTA)

**Mheshimiwa Spika,** COSOTA inajukumu kubwa la kuhakikisha kuwa haki za wasanii zinapatiwa ulinzi unaostahili ili waweze kunufaika na jasho lao. Ili kufikia lengo hili Sheria ya Hakimiliki na Haki Shiriki Na. 7/1999 hainabudi kufanyiwa marekebisho. Kamati imearifiwa kuwa marejeo yanaendelea kufanyika yakihusisha nyaraka na jedwali la maoni ya marekebisho ya sharia. Aidha tayari waraka wa marekebisho ya sheria umeandaliwa na hatua itakayofuata ni kuwasilishwa kwenye Kikao cha Baraza la Mawaziri. Ushauri wa Kamati ni kuwa kazi hii ikamilike kwa haraka hasa ikizingatiwa kuwa wimbi la wizi wa kazi za wasanii ni kubwa sana hapa nchini, na ulinzi wa kazi za wasanii haujakuwa mzuri vyakutosha.

**Sambamba na jitihada hizi Kamati inashauri** COSOTA kuwa na mkakati mahsusi wa kushirikiana kwa karibu zaidi na Wadau wote muhimu katika tasnia ya sanaa kama Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Wasanii na vyombo huru vya wasanii, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu Tanzania, Jeshi la Polisi, na Makampuni ya usambazaji na uzalishaji wa kazi za sanaa. Kuwepo kwa ushirikiano wa karibu wa aina hii kutarahisishaupatikanaji wa taarifa muhimu zitakazowezesha kufanyika kwa ufazisi zaidi ukaguzi wa bidhaa na ulinzi wa haki miliki nchini.

## *3.6* BODI YA LESENI YA MAGHALA (TWLB)

**Mheshimiwa Spika,**Bodi imeendelea kusimamia utekelezaji wa mfumo wa Stakabadhi za Maghala katika maeneo yote yanayayotekeleza mfumo huo nchi nzima. Jumla ya Leseni 18 zilitolewa kwa Waendesha maghala,

Leseni 21 za maghala na Leseni 2 kwa Kampuni za ukaguzi wa maghala. Katika kuhakikisha kuna ufanisi katika mfumo huu Bodi imefanya ukaguzi wa maghala yote 21 yaliyosajiliwa na kupewa leseni mwaka 2014/2015 na kusambaza vitabu 259 vya stakabadhi kwa waendesha maghala kwenye mazao ya korosho, kahawa na mpunga ikilinganishwa na vitabu 206 mwaka 2013/2014.

**Mheshimiwa Spika**, Tani zipatazo 176,000 za korosho ziliuzwa kupitia mfumo katika msimu wa 2014/2015 ukilinganisha na tani 129,460 msimu wa 2013/2014 ikiwa ni ongezeko la tani 46,540. Aidha, katika mwaka 2014/2015 tani 7,654.8 za kahawa ziliuzwa ukilinganisha na tani 5,207 za kahawa zilizouzwa katika msimu wa 2013/2014.

**Mheshimiwa Spika, Bodi k**utokana na usimamizi thabiti bei za mazao inayofanya , bei zimezidi kuimarika. Aidha, korosho imeuzwa kati ya shilingi 1,440/ kg – 2,200/ kg ikilinganishwa na kati ya shilingi 1,402 /kg – 1,723 /kg Msimu wa 2013/2014, bei ya kahawa isiyokobolewa iliongezeka na kufikia wastani wa shilingi 6,800 /kg msimu wa 2014/2015.

## *3.7* SHIRIKA LA UTAFITI NA MAENDELEO YA VIWANDA TANZANIA (TIRDO)

**Mheshimiwa Spika,** Shirika linafanya tafiti zenye lengo la kupata teknolojia bora za uzalishaji na zenye tija kwa viwanda kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Sayansi na

Teknolojia (COSTECH) imepeleka wataalamu wawili (2) wa nishati, mtaalam mmoja (1) wa chakula na mtaalam mmoja (1) wa mazingira katika viwanda vya ngozi kusoma nchini India ili kufanya tafiti za makaa ya mawe, namna ya kukabiliana na uchafuzi wa mazingira na pia katika uzalishaji wa bidhaa za chakula hapa nchini.Tafiti hizi zitalenga kurahisisha upatikanaji wa nishati ya makaa ya mawe kwa matumizi ya viwanda vikubwa na vidogo, biashara, na pia majumbani.

**Mheshimiwa Spika**, tafiti hizi zitasaidia kutafuta njia mbadala za matumizi ya mabaki (wastes) yanayotokana na uzalishaji viwandani. Tayari COSTECH wametoa kasma ya kununua baadhi ya vifaa vitakavyotumika kwenye tafiti hizi. Sambamba na hilo Shirika lilifadhiliwa na taasisi ya kimataifa ya utafiti (International Development Research Centre (IDRC)) ya Canada kufanya utafiti wa kuainisha manufaa na changamoto za watafiti na wavumbuzi wa taasisi za Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,**Shirika kwa kutumia fedha zake za ndani linajenga maabara (*ICT Lab*). Maabara hiyo imekamilika kwa asilimia tisini (90%) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 24 kwa wakati mmoja. Aidha, Shirikalimeandaa mtaala wa kufundishia na kuuwasilisha Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) pamoja na Wakala ya Serikali Mtandao (eGA) kupata maoni na limeingia makubaliano ya ushirikiano (MOU) kati yake na Mzinga Cooperation katika maeneo mbalimbali ikiwemo eneo la 'Cyber Security'.

**Mheshimiwa Spika**, Shirika limeendelea na mchakato wa mpango wa matumizi bora ya ardhí ya TIRDO (*land use plan*). Shirika limeshapata ridhaa ya Msajili wa Hazina kwa utekelezaji. TIRDO imeandaa miradi itakayotekelezwa katika Mpango huo. Miradi itatekelezwa kwa ushirikiano na Sekta Binafsi yaani *public – private partnership*.

**Mheshimiwa Spika,**Miradi imewasilishwa Kituo cha Uwekezaji (TIC) kwa ushauri kulingana na sheria ya uwekezaji. TIC na TIRDO zimekubaliana atafutwe mshauri mwelekezi kufanya maboresho katika andiko la miradi hiyo (*Business Plan*) ili TIRDO iweze kuendelea na mchakato wa kutangaza na kupata wawekezaji. TIC bado wanaendelea na uchambuzi na TIRDO imewaandikia barua kama njia ya kufuatilia suala hilo.

**Mheshimiwa Spika,**TIRDO imeendelea na mkakati wa kuimarisha Sekta ya ngozi. Shirika limenunua mtambo wa kuchakata taka za ngozi (leather recycling machine). Hatua ya usimikaji imekamilika kwa zaidi ya asilimia tisini (90%) na mtambo huu utatumika kuwapa mafunzo wadau wote wa ngozi nchini jinsi ya kuongeza thamani kwenye taka za ngozi (leather trimmings).

**Mheshimiwa Spika**, Shirika katika kuendelea na ukamilishaji wa mchakato wa kuhakiki (Accreditation) na kuboresha maabara ya mazingira na ya vifaa vya kihandisi, ili ziweze kufikia viwango vya kimataifa kuweza kutoa

huduma bora kwa wazalishaji viwandani nchini.Shirika limeweza kuandaa maombi na kuwasilisha taasisi ya uhakiki ya Southern African Development Community Accreditation System (SADCAS) kupata uhakiki wa maabara ya mazingira. Ili kufanya uhakiki kikamilifu Shirika limenunua 'adaptors' kwa ajili ya upimaji (*proficiency testing*). Kwa sasa maabara inaendelea kufanya *calibration ya Gas Analyser*ili kuweza kuendelea na zoezi la upimaji kwa ustadi (*Profiency testing*).

**Mheshimiwa Spika**, Shirika limeendelea kushiriki katika shughuli za mfumo wa kuhakiki wa matokeo ya upimaji kwa ustadi (*Profiency testing*) wa hewa ili kuweza kutoa matokeo yenye uhakika Zaidi yanayozingatia viwango vya kimataifa (ISO /IEC 17025).

**Mheshimiwa Spika,**Kwa upande wa maabara ya vifaa vya kihandisi – *Non Destructive Testing* (NDT) tayari Shirika limetayarisha na kufanya mapitio ya maandiko ya utendaji kazi wa kitaalamu (*Standard Operating Procedures*) kwa kutumia mionzi (*Radiographic testing method)*

**Mheshimiwa Spika,**Shirika limeendelea kuisaidia kampuni ya GS1 kutekeleza miradi yao kitaalamu iweze kuendelea kutoa nembo za mistari kwa makampuni ya ndani na nje ya nchi pamoja na kuendelea kufanya uhamasishaji kuhakikisha kampuni nyingi zaidi zinapata nembo za mistari kutoka GS1. Kufikia mwezi Aprili, 2015,

jumla ya bidhaa 13,750 zimepatiwa nembo za mstari na kampuni 815 zimekuwa wanachama wa GS1 hapa nchini, kati ya hao kampuni nne (4) ni kutoka nje ya Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, Shirika limeendelea kukamilisha mchakato wa kurejea Sheria ya Bunge Na. 5 ya mwaka 1979 iliyoanzisha TIRDO kwa kuwasilisha ripoti ya mapitio ya sheria kwa Wizara mama (Wizara ya Viwanda na Biashara) na hatimaye kupelekwa Bungeni kati ya mwezi Aprili na Julai 2015.Aidha, Shirika hadi sasa halina Baraza tangu mwaka jana na hivyo hali halisi ya mapitio ya sheria bado haijabadilika kwa kuwa ripoti haijawasilishwa kwenye Baraza ambayo ndio hatua ya mwisho kabla ya kuwasilishwa wizarani.

**Mheshimiwa Spika,**Shirika limeweza kuingia makubaliano ya kiushirikiano (MOU) kati yake na Benki ya TIB Development kwa ajili ya utekelezaji wa kazi mbalimbali ikiwemo ya kutoa tathmini za kitaalam kwa wawekezaji wakubwa na wadogo. Tayari vikosi kazi viwili vimeshaundwa kwa ajili ya kuanza mchakato wa kutekeleza ushirikiano huo.

**Mheshimiwa Spika**, Shirika limetoa huduma za kitaalamu katika jumla ya viwanda vitano(5) katika mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Morogoro na Tanga lengo likiwa ni kuongeza uzalishaji wa bidhaa bora bila kuchafua mazingiza; pia zinazolenga matumizi bora ya nishati. Shirika limeandaa maandiko ya miradi (project proposals) na kuyawasilisha kwa wadau mbalimbali wakiwemo

*Confederation of Tanzania Industries (CTI)* na Mamlaka ya Maji Dar es Salaam (DAWASCO). Lengo la CTI ni kuvinufaisha viwanda na wadau wanachama kuongeza ufanisi wa nishati na pia kupunguza gharama za uendeshaji. Majadiliano kati ya wadau hao na Shirika yanaendelea ili kuwezesha kuanza kwa miradi hii.

## *3.8* KITUO CHA ZANA ZA KILIMO NA TEKNOLOJIA VIJIJINI (CAMARTEC)

**Mheshimiwa Spika,** Kituo kinaendelea na jukumu lake la kubuni na utengenezajiwa teknolojia za kuongeza tija na kupunguza aharubu katika kilimo vijijini. Aidha,Kituo kinaendelea kurekebisha Sheria iliyoanzisha CAMARTEC ili kukidhi matakwa mapya.Kazi ya kurekebisha sheria inaendelea na itakamilika mara baada ya kupatikanakwa fedha.

**Mheshimiwa Spika,**Kituo kinajenga mitambo mikubwa ya biogesi kwa ajili ya kufua umeme kwenye shule na taasisi nchini kwa kuanzia na Mikoa ya Manyara, Mara, Kagera na Mwanza.Upembuzi yakinifu umekwishafanyika katika baadhi ya magereza yaliyopo mkoani Mwanza na Mara na utekelezaji wake utaanza pindi fedha za utekelezaji wake zitakapopatikana.

**Mheshimiwa Spika,**Kituo kinaendelea kueneza vifaa vya matumizi ya nishati ya biogesi (biogas appliances) katika maeneo kulikojengwa mitambo ya biogesi ili kuifanya teknolojia hiyo kuwa endelevu. Aidha, Taa, Majiko, Bomba

la kutolea gesi na vifaa vyake vimeendelea kutolewa katika maeneo yote ya Kilimanjaro, Tanga, Manyara, Arusha, Singida, Mbeya, Mwanza, Mara na maeneo mengine ambayo kituo kimejenga mitambo ya biogas kupitia mradi wa Tanzania Domestic Biogas Programe (TDBP).

**Mheshimiwa Spika,** Kituo kimetoa mafunzo kwa wajasiriamali juu ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu na usanifu wa mitambo ya biogesi. Maeneo yote ya mikoa ya Kilimanjaro, Mara, Shinyanga, Mbeya, Mwanza na sehemu nyingine ambazo kituo kimekuwa kikijenga mitambo ya biogesi kupitia mradi wa *Tanzania Domestic Biogas Programe* (TDBP) kimeendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali juu ya ujenzi na usanifu wa mitambo ya biogesi.

## *3.9* SHIRIKA LA MAENDELEO YA VIWANDA VIDOGO NA BIASHARA NDOGO (SIDO)

**Mheshimiwa Spika**, Shirika la SIDO lina kazi ya kujenga uwezo wa vituo vya maendeleo ya teknolojia ya SIDO kuzalisha mashine ndogo zitakazotumika katika uongezaji thamani mazao ya kilimo hasa vijijini. Katika mwaka 2014/2015 SIDO ililenga kuhakikisha kuwa nyenzo zote zinazotakiwa katika kuanzisha viwanda vidogo zinapatikana kwa ajili ya matumizi ya wajasiriamali.

**Mheshimiwa Spika**, SIDO hutafuta teknolojia kutoka sehemu mbalimbali, hutumia nyenzo zilizopo kuzifanyia

marekebisho ili ziendane na hali halisi ya mazingira zinamotumika. Aidha, Shirika linasimamia vituo vya maendeleo ya teknolojia ndani ya mitaa ya viwanda vidogo vilivyoanzishwa ili viweze kubuni, kutengeneza na hatimaye kuuza bidhaa au mashine mbalimbali kwa wananchi na kuwaelekeza namna nzuri ya kuzitumia na kuanzisha miradi.

**Mheshimiwa Spika**, Vituo hivyo vinavyozalisha teknolojia ni pamoja na Arusha (mashine za kukamua miwa na zana za kilimo), Iringa (mashine za mbao na usindikaji wa mtama), Kigoma (mashine za kusindika mawese na mazao ya mchikichi), Kilimanjaro (mashine za kutengeneza chaki na bidhaa za ujenzi), Lindi (mashine za kusindika korosho na mihogo), Mbeya (mashine za usindikaji wa maziwa na zana zinazolenga kupunguza uharibifu wa mazingira) na Shinyanga (mashine za kusindika ngozi na kutengenezea bidhaa za ngozi). Huduma zilizotolewa zimewezesha uzalishaji na hatimaye upatikanaji wa bidhaa mbalimbali za viwanda vidogo mijini na vijijini.

**Mheshimiwa Spika,**Katika mwaka 2014/15 jumla ya teknolojia mpya 20 zimetafutwa kutoka ndani na nje ya nchi kwa ajili ya matumizi ya miradi ya uzalishaji. Jukumu hili limetekelezwa kwa kutengeneza na kusambaza mashine mpya za aina mbalimbali 155 kupitia vituo vya kuendeleza teknolojia vilivyopo mikoa ya Arusha, Iringa, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Mbeya na Shinyanga. Kati ya teknolojia mpya zilizosambazwa ni pamoja na za

utengenezaji wa sabuni, usindikaji wa maziwa, matunda, tangawizi, mafuta ya kula, asali na utengenezaji wa misumari . Teknolojia hizo zimesaidia kuongeza tija, kuimarisha na kuongeza ubora wa bidhaa za wajasiriamali.

## *3.10* WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI (BRELA)

**Mheshimiwa Spika,**Katika kurahisisha upatikanaji wa taarifa na huduma Wakala inaweka mifumo ya kiteknolojia itakayowawezesha wadau kupata hizo kwenye mifumo ya kompyuta (On line registration systems) kwa wakati.Aidha,Wakala imeboresha mifumo ya usajili na utunzaji wa masijala kwa kuweka mifumo ya kielektroniki saidizi kwa ajili ya kutunza masijala na usajili wa majina ya biashara ambao mifumo hiyo imewezesha kusajili jina la biashara ndani ya masaa manane (8) tu badala ya siku 1 mpaka 3 za awali. Sambamba na jitihada hizi Kamati inashauri kufanyiwa kazi kwa haraka mapendekezo **ya** Mshauri Elekezi aliyeajiriwa kwa ajili ya kupitia taratibu za usajili na kuziboresha (*Business Process Mapping and Re-engineering*) na kuandaa mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao (*Online Registration System Design)*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imearifiwa kuwa BRELA imeendelea kufanya maboresho ya Sheria inazozisimamia ambapo Sheria ya Makampuni Sura 212 ya Sheria za Nchi (*The Companies Act, Cap. 212*) na Sheria ya Uandikishaji wa Majina ya Biashara Sura 213 ya sheria za nchi (*The Business Names (Registration) Act, Cap. 213*) zimefanyiwa

marekebisho na kupitishwa na Bunge. Rasimu ya Kanuni (*Regulations*) kwa ajili ya sheria kuanza kutumika zimeandaliwa na kupitishwa na Wizara ya Viwanda na Biashara, na sasa kanuni hizo zipo kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Lengo la maboresho hayo ni kurahisisha mazingira ya utoaji wa huduma za usajili wa biashara nchini.

## 3.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

**Mheshimiwa Spika,** sekta ya Viwanda na Biashara imeendelea kuchangia Uchumi hasa katika shughuli za uzalishaji, usindikaji usambazaji na masoko. Sekta hizi bado zina nafasi kubwa ya kuliwezesha Taifa kuondokana na umaskini na kulifikisha katika kiwango cha uchumi wa kati wa Viwanda. Haya yote yanawezekana ikiwa Serikali itaweza kusimamia ipasavyo na kuratibu shughuli zote za msingi zinazohusu sekta hizi na kukabiliana na changamoto zifuatazo:-

**3.2 Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Exporting Processing Zones (EPZ) imeendelea kuhamasisha uwekezaji pamoja na ujenzi wa baadhi ya miundombinu katika maeneo ya EPZ/SEZ. Pia imeendelea kutoa fidia katika maeneo maalum ya uwekezaji mfano eneo la Kurasini ili kutekeleza mradi wa Tanzania-China Logistics Centre na eneo la mradi wa EPZ – Bagamoyo. Maeneo haya ni ya kimkakati yaliyopewa kipaumbele kwenye utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa ; na hivyo yanategemewa kuongeza ajira, soko la malighafi nchini pamoja na kuvutia uwekezaji na biashara.

**Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji wa zoezi hili la ulipaji wa fidia umekuwa wa kusuasua na hivyo kuondoa ile dhana

kuwa ni kweli Miradi ya Kimkakati. Kamati inaona kuwa kwa mwenendo kama huu wa utoaji hafifu wa fedha kwenye miradi tuliyoipa kipaumbele kwenye Mpango wa Maendeleo ya Taifa kamwe hatutaweza kuimaliza kama tulivyopanga.

Aidha, Kamati inatahadharisha kuwa upo uwezekano mkubwa wa kuwapoteza wawekezaji/wadau wa maendeleo kwenye miradi mikubwa kama hii ambayo tuliwahihikishia kushirikiana nao ipasavyo. Ni vyema kama Taifa tukawa na uelewa ulio sawa kuwa Dunia ya sasa ni ya kiushindani na kibiashara na muda haupo upande wetu, kila nchi inapenda kupata fursa za kuingia ubia kama hizi za kwetu na zinajitahidi kuweka mazingira wezeshi ya kupata wawekezaji; tusichezee ursa hizi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha inalipa fidia katika maeneo yote yaliyofanyiwa tathmini yaliyopo chini ya EPZ na SEZ kufikia Mwaka wa Fedha 2015/2016; yenye gharama iliyofikia Shilingi Bilioni 60. Aidha, kwakuwa bajeti iliyowasilishwa na Wizara kwa ajili ya fidia ya maeneo haya ni Shilingi 26 bilioni tu, Kamati inatoa rai kuwa ni vyema Serikali ikatenga Shilingi Bilioni 60 katika fengu hili ili fidia yote iweze kulipwa kwa mkupuo kwa mujibu wa tathmini. Ikumbukwe kuwa tathmini hizi zimefanyika muda mrefu tangu mwaka 2008, na kwamba wananchi wamesubiri kwa muda mrefu kupata haki yao ya fidia; na kwa kuchelewa huku gharama zimekuwa zikiongezeka kila mwaka na kuongeza mzigo kwa Taifa. Ni vyema serikali ya awamu ya Nne ikamaliza hatua hii ya ulipaji fidia hii ili Serikali ya awamu ya Tano iingie kwenye utekelezaji wa Miradi.

**3.3 Mheshimiwa Spika**, uzoefu unatuonyesha kuwa nchi nyingi Duniani zinalinda viwanda vyao vya ndani pamoja

ya kuwa kuna ushindani. Lazima tuhakikishe viwanda vyetu vinazalisha na kutosheleza soko la ndani na la nje kwa kutumia malighafi tunayozalisha nchini. Kwa kuzingatia haya Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

i) Serikali iongeze jitihada za kufufua Kiwanda cha General Tyre (EA) ltd ikiwemo ukamilishaji ukarabati wa umeme wa awamu ya tatu;
ii) ukarabati wa mitambo na kufanya majaribio ya uzalishaji wa matairi ufanyike mapema;
iii) kwakuwa kiwanda hiki kimekuwa na mgogoro kwa muda mrefu, Serikali ifanye jitihada za makusudi kukamilisha taratibu za manunuzi ya hisa asilimia 26 kutoka kwa mbia wa zamani Continental AG ili kuiwezesha NDC kuendelea kutafuta wabia wenye uwezo na uzoefu wa uzalishaji wa matairi ya magari ili uzalishaji uweze kuanza. Hii itasaidia kuongeza ajira, wigo wa ukusanyaji mapato yatokanayo na kodi na pia kusaidia kukuza uchumi,
iv) Miradi yote inayotekelezwa kupitia Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) yaani mradi wa makaa ya mawe wa Mchuchuma

v) na wa Chuma cha Liganga, mradi wa kuzalisha umeme wa Ngaka; na mradi wa kutengeneza Viuadudu (Biolarvicides) vya kuua viluwiluwi vya mbu wa malaria na ule wa uchimbaji wa magadi (Soda Ash) –Ziwa Natron; isimamiwe na kuratibiwa vizuri ili ikamilike kwa wakati uliopangwa. Kukamilika kwa miradi hii sambamba na kujenga uwezo wa Wizara wa kuandaa Sera ya Maendeleo ya Viwanda na Kuboresha Utendaji wa Viwanda kutasaidia kupatikana kwa umeme wa uhakika, ajira na kuongeza mapato na hivyo kusaidia kukuza uchumi kupitia sekta ya viwanda.
vi) Kwa mradi wa kuzalisha umeme wa upepo Singida, Kamati hairidhishwi na kusuasua kwa mazungumzo ya Mkataba wa Mkopo (Loan Agreement) kati ya Wizara ya Fedha na Benki ya EXIM; na inasikitishwa zaidi kutokana na ukweli kuwa ucheleweshaji huu unaofanyika ndani ya Serikali yenyewe.

Ikumbukwe kuwa utekelezaji wa mradi huu ni wa mwaka mmoja tu na utaweza kuingiza megawati za kutosha katika Gridi ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kusimamia ipasavyo ujenzi wa viwanda vipya vya Saruji na hivyo kuleta matumaini ya kuongeza uwezo wa uzalishaji wa Saruji nchini na upatikanaji wa ajira mpya. Kukamilika kwa ujenzi wa viwanda vipya vya saruji yaani Dangote Cement Obajan Plant cha Mtwara, Athi River Cement Co. – Tanga, Mbagala Cement Co.- Dar es Salaam na Arusha Cement Co.- Arusha kutasaidia upatikanaji zaidi wa saruji na hivyo kuachana na tabia ya kuagiza saruji toka nje inayouzwa kwa bei ya chini kutokana na ruzuku inayotolewa kwa viwanda vyao na hivyo kupelekea viwanda vyetu kujiendesha katika ushindani usio wa haki. Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua za kutoza kodi au ushuru

kwenye saruji inayoagizwa toka nje ili kulinda uzalishaji wa ndani.

**Mheshimiwa Spika,** viwanda vya sukari vilivyopo nchini pamoja na vile vidogo kwa ujumla vinazalisha takribani tani 304,000 na mahitaji yetu ni tani 400,000. Jitihada za makusudi zinahitajika kuongeza uzalishaji ili kuweza kukidhi mahitaji ya ndani. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaongeza ujenzi wa viwanda vipya vya sukari sambamba na kongeza kilimo cha miwa ili kutosheleza mahitaji na kulinda bei za walaji na hivyo kuondokana na utaratibu wa kuagiza sukari toka nchi za nje

**Mheshimiwa Spika**, Shirika la Viwango la Taifa (TBS) limekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha linadhibiti uingizaji wa bidhaa zisizo bora na hivyo kukuza matumizi ya viwango na hivyo kulinda afya ya walaji, usalama wa walaji na kulinda mazingira ya nchi yetu. Hata hivyo,

Kamati imebaini kuwa pamoja na juhudi hizi, Shirika linakabiliwa na changamoto kubwa ya upungufu mkubwa wa wafanyakazi. Itakuwa ni miujiza kutegemea idaya iliyopo sasa ya wafanyakazi 222 waweze kufanya kazi na kuzunguka Tanzania nzima kuhakikisha kuwa bidhaa zenye ubora unaokubalika tu ndio zinatengenezwa au kuingizwa nchini na zinakidhi viwango vya kimataifa.

Wakati Kamati inafanya zoezi la kupitia taarifa ya Wizara, Serikali iliahidi kulifanyia kazi ombi la muda mrefu la TBS ili kibali cha kuajiri wafanyakazi wapatao 336 kiweze kutolewa. Kamati inamtaka Wazili kulieleza Bunge lako kuwa mchakato wa kibali cha kuajiri wafanyakazi wapya kimefikia wapi.

**Mheshimiwa Spika,**Viwanda vidogo vinauwezo wa kutoa mchango mkubwa kwa ukuaji uchumi wa nchi yetu. Hata hivyo ili viwanda hivi viweze kutoa mchango wake kikamilifu kwa ukuaji wa uchumi, lazima yawepo mazingira wezeshi yatakayosaidia viwanda hivyo kufanya kazi kwa ufanisi. Nchi kama India imefanikiwa kuwa na sekta madhubuti ya viwanda vidogo kutokana na kuweka mazingira wezeshi. Leo hii sekta ya viwanda vidogo nchini India inachangia sana katika kutoa ajira; ikizidiwa tu na sekta ya kilimo.

Kwa upande wetu hapa nchini, uzoefu unaonesha kuwa pamoja na kuwa kilimo ndicho kwa muda mrefu kimeongoza katika utoaji wa ajira kwa watanzania; viwanda navyo vimekuwa vikibeba mzigo wa changamoto ya ajira mijini, changamoto ambayo inatokana na wimbi la ongezeko la watu wanaokimbilia mijini. Hata hivyo, kufuatia kufungwa kwa viwanda vingi; mzigo huo sasa unabebwa na sekta isiyo rasmi.

Ili kuweka uwiano mzuri utakao tuhakikishia kuongezeka kwa uzalishaji kupitia kilimo, kuongezea mazao yetu thamani, na kuondoa tatizo la ajira; ni vyema tukaangalia uwezekano wa kuvutia uwekezaji wa viwanda nchini kwa kuingiza teknolojia ya viwanda vidogo na vya kati ambavyo vilishamiri katika nchi za Asia; lakini kwasasa vinafungwa kutokana na kupanda kwa gharama za uzalishaji katika nchi hizo. SIDO ambayo imefanya kazi kubwa katika kuendeleza viwanda vidogo nchini, iwezeshwe kifedha na kushirikishwa kikamilifu katika kusimamia uingizwaji wa teknolojia na uanzishwaji wa viwanda hivi.

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya maziwa inafursa kubwa ya kuchangia katika kukuza uchumi wa nchi yetu. Tanzania tunafursa kubwa ya kukuza uchumi na kuwaondolea wananchi umasikini. Tuna viwanda vya kusindika maziwa 82. Uwezo wa viwanda kuzalisha kwa siku ni lita 64/08 na uzalishaji halisi wa viwanda kwa siku ni lita 167,070 sawa na 26%. Hata hivyo, kama Taifa bado hatujaitumia vyema fursa hii

kutokana na mazingira mabovu yaliyopo, ambayo yamezuia ukuaji wa sekta ya maziwa. Takwimu zinaonesha kuwa wakati ambapo Tanzania ni nchi ya tatu Afrika kwa wingi wa mifugo; kwa kuwa na Ng'ombe wapatao milioni 21.3, na kuzalisha kiasi cha lita za maziwa zipatazo milioni 5, ni lita 112,500 tu ndizo zinasindikwa. Chakushangaza zaidi ni kwamba ni 3% ya maziwa yanayozalishwa nchini ndiyo yanaingia katika soko rasmi ikilinganishwa na 30% Kenya na 7% nchini Uganda.

**Mheshimiwa Spika,** Viwanda vyetu vya usindikaji wa maziwa vimekuwa vikitumia sehemu ndogo ya uwezo wake kusindika kwa takriban 26.7% tu, wakati ambapo viwanda vya Kenya vinatumia 85.7% na Uganda 45.5% ya uwezo. Kwa hali hii usindikaji Tanzania unatoa bidhaa chache za maziwa ikilinganishwa na nchi jirani hivyo kuathiri uwezo wa usindikaji na kiushindani kwenye soko la EAC. Mojawapo ya sababu zinazochangia hali hii ni gharama kubwa za uzalishaji wa bidhaa hizi nchini ikilinganishwa na nchi jirani. Utafiti uliofanywa na*RLDC (2010)* unaonesha gharama za kusindika Maziwa (Pasturized milk) kwa lita moja kwa kiwanda kilichopo Tanzania inagharimu kiasi cha Tsh. 778 ikilinganishwa na Tsh. 526 kwa Kenya. Aidha, takwimu zitokanazo na utafiti huu zinaonyesha kuwa tuna changamoto kubwa kwani lita nyingi za maziwa hazikusanywi toka kwa wafugaji na kusindikwa.

**Mheshimiwa Spika, T**akwimu zinaonesha vilevile kuwa kiwango cha unywaji wa maziwa Tanzania ni kidogo sana. Kwa wastani mtanzania anakunywa lita 40 tu za maziwa kwa mwaka ikilinganishwa na lita 100 kwa mkenya, na lita 55 kwa mganda. Aidha, changamoto nyingine inayodumaza ukuaji wa sekta ya maziwa nchini ni mfumo wetu wa kodi kwa bidhaa za maziwa na maziwa yaliyosindikwa (VAT 18%); mfumo ambao hautoi ushindani ulio sawa ikilinganishwa na majirani zetu wa Kenya ambao katika kuifanya sekta ya maziwa kuwa competitive, mwezi Machi mwaka huu ilipitisha uamuzi wa kutotoza kabisa kodi katika bidhaa za maziwa na maziwa yaliyosindikwa.

Ili Taifa linufaike na fursa zilizopo katika sekta ya maziwa nchini, ni lazima kama Taifa tuhakikishe tunakuwa na

mkakati wa kuvilinda viwanda vichache vilivyopo ili viweze kushindana na viwanda vya nchi jirani. Aidha, lazima tuje na mkakati wa kuongeza idadi ya viwanda vya kuyasindika maziwa yetu hapa nchini; na vilevile kuwahamasisha wananchi kujenga utamaduni wa kunywa maziwa. Kwa kufanya hivi tutapunuza tatizo la ajira na kuongeza kipato cha watu wetu.

**Mheshimiwa Spika, e**neo linguine ambalo kama Taifa hatujaweza kulitumia kikamilifu katika kukuza pato la Taifa ni katika **sekta ya uvuvi**. Sekta hii inafursa kubwa sana ya kuweza kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu katika nyanja za kukuza pato la wananchi, ajira, na hata katika kuboresha lishe na usalama wa chakula kwa watu wetu. Ili sekta hii iweze kutupatia mchango mkubwa kiuchumi ni vyema sasa tukawa na mkakati unaotoa miongozo ya uwekezaji wa kibiashara katika sekta hii (**Investment Policy forAquaculture Parks**); mkakati ambao utatuwezesha kuingia katika **ufugaji wa samaki kisasa** kwa kuanzisha maeneo maalum ya biashara ya ufugaji wa samaki **(Aquaculture Value Chain Parks).**

**Mheshimiwa Spika, u**anzishaji wa maeneo maalum ya biashara ya ufugaji wa samaki (**Aquaculture Value Chain Parks)** utatusaidia kuongeza kwa haraka mchango wa sekta ya uvuvi katika uchumi wa nchi yetu. Hii inatokana na ukweli kuwa 46% ya samaki wanaopatikana katika soko la Dunia wanapatikana kupitia ufugaji wa samaki katika bahari ya kina kifupi, mabwawa na mito. Jirani zetu wa Uganda, Kenya na Rwanda tayari wamepiga hatua kubwa

katika hili. Wakati ambapo mauzo ya samaki nchini Uganda yanafikia tani 550,000 kwa mwaka, kati ya hizo, tani 90,000 zinatokana na ufugaji wa samaki. Hii inaifanya Uganda kuwa nchi ya tatu katika Afrika kwa ufugaji wa samaki ukiziacha Misri na Naijeria. Uganda kwa sasa wanakusudia kuongeza idadi ya samaki wanaotokana na ufugaji hadi kufikia tani 300,000 ifikapo 2016.

**Mheshimiwa Spika, h**adi sasa idadi kubwa ya Watanzania hawajafaidika na mikakati mbalimbali ya Serikali ya kuwawezesha kiuchumi.Ili lengo la kuwasaidia na kuwawezesha wananchi wengi wenye kipato cha chini liweze kufikiwa lazima **targeting** nautekelezaji wa mikakati hii isimamiwe ipasavyo. Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wafanyabiashara Wadogo ***(NEDF)*** unaosimamiwa na**SIDO,** mtaji wake ni mdogo sana kuweza kutosheleza mahitaji ya wananchi. Ni vyema Serikali ikaangalia uwezekano wa kuongeza mtaji katika mfuko huu.

## 13.0 HITIMISHO:

**Mheshimiwa Spika,**Kamati inapenda kumshukuru Waziri waViwanda na Biashara Dkt. Abdallah Omar Kigoda (MB), Katibu Mkuu, pamoja na wataalamu wa Wizara ya Viwanda

na Biasharakwa kuwa tayari kutoa ufafanuzi na kupokea maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati yangu wakati wote wa mjadala wa makadirio haya. Ni matarajio ya Kamati kuwa ushirikiano huu utaendelea katika mwaka ujaowa Fedha.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biasharaambao wameweza kutoa maoni na michango ya mawazo yao mbali mbali katika kuboresha makadirio haya ili hatimaye yaletwe mbele ya Bunge hili tukufu. Naomba nitumie nafasi hii kuwatambua wajumbe wote kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Luhaga Joelson Mpina,MB, Mwenyekiti
2. Mhe. Dunstun Luka Kitandula,MB, M/M/Kiti
3. Mhe. Margareth Agness Mkanga, MB, Mjumbe
4. Mhe. Aieshi Khalfan Hilary, MB, Mjumbe
5. Mhe. Ester Lukago Minza Midimu,MB, Mjumbe
6. Mhe. Hussein Nassor Amar , MB Mjumbe
7. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, MB, Mjumbe
8. Mhe. Joyce John Mukya, MB, Mjumbe
9. Mhe. David Zakaria Kafulila, MB, Mjumbe
10. Mhe. Shawana Bukhet Hassan, MB, Mjumbe
11. Mhe. Said Mussa Zubeir, MB Mjumbe
12. Mhe. Vicky Pascal Kamata, MB Mjumbe

13. Mhe. Naomi Ami Mwakyoma Kaihula,MB Mjumbe

14. Mhe. Khatibu Said Haji, MB Mjumbe

15. Mhe.Freeman Aikael Mbowe, MB Mjumbe

16. Mhe. Josephine Jonson Genzabuke, MB Mjumbe

17. Mhe. Eng. Habib Juma Mnyaa, MB Mjumbe


18. Mhe. Mohamed Hamis Misanga , MB Mjumbe

19. Mhe. Dkt Terezya Luoga Huvisa, MB Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, naomba nikushukuru sana wewe mwenyewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kutupatia maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah.Halikadhalika, napenda kuwashukuru NduguAngela Shekifu, Ndugu Rachel Nyega na Ndugu Grace Samwelkwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato naMatumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara, Fungu 44, yenye maombi ya jumla ya Shilingi **116,496,769,000** Kati ya fedha hizo shilingi **53,697,588,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **62,799,181,000/=** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

*Kielelezo Na. 11: Mgawanyo wa bajeti ya Wizara kati ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi ya Maendeleo kwa mwaka 2015/2016*




**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**Mhe. Dunstan L. Kitandula Mb.**

**MAKAMU MWENYEKITI**

**KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA**